Tahadhari
Badilika ukomeshe
Ghasia za Kijinsia

KIJITABU CHA MAELEZO
Swahili Version

Imechapishwa na Ubia wa Wakimbizi nchini Kenya, Refugee Consortium of Kenya kwa ufadhili wa European Union Humanitarian Aid

Co-funded by
European Union
Humanitarian Aid

RCK
REFUGEE CONSORTIUM OF KENYA

Tahadhari
Badilika ukomeshe
Ghasia za Kijinsia

KIJITABU CHA MAELEZO

Imechapishwa na Ubia wa Wakimbizi nchini Kenya, Refugee Consortium of Kenya kwa fadhili wa United Nations Trust Fund

Yaliyomo

Utangulizi **7**

Dhana muhimu **8**

Ghasia za Kijinsia ni Nini? **10**

Aina za Ghasia za Kijinsia 10

Ghasia za kimapenzi 10

Ghasia za kimwili 10

Ghasia za kihisia na kisaikolojia 10

Ghasia za kijamii na kiuchumi 11

Mila za kitamaduni zinazosababisha madhara 11

Ukeketaji wasichana 11

Wakimbizi nchini Kenya wanalindwa vipi kutokana na ghasia za kijinsia? **12**

Ghasia za kimapenzi – Watu wazima 12

Ubakaji 12

Jaribio la ubakaji 12

Shambulio la nguvu la kimapenzi 12

Vitendo vya kuaibisha vilivyolazimishwa au kushawishiwa (Sehemu ya 6 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006) 13

Vitendo vinavyosababisha kuingilia kingono au vitendo vya kuaibisha mbele ya familia, watoto au wale wenye ulemavu wa kiakili (Sehemu ya 7 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006) 13

Unajisi wa watu wenye akili pungufu na mazuzu (Sehemu ya 146 ya Utaratibu wa Adhabu) 13

Vitendo vya kuaibisha na watu wazima 13

Bugudha za kimapenzi 14
Kuambukiza kimakusudi virusi vya ukimwi (HIV) au magonjwa ya zinaa yanayotishia maisha 14
Kusambaza magonjwa 14
Majaribio ya kumtoa mimba mtu mwingine 14
Ghasia za kimapenzi – Watoto.....15
Unajisi 15
Jaribio la Kunajisi 15
Njama ya Kunajisi 15
Kitendo cha kuaibisha na mtoto 15
Unyanyasaji wa Kimapenzi – Watu wazima 17
Unyanyasaji wa Ukahaba (Sehemu ya 17 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006) 17
Ukahaba wa watu wenye ulemavu wa kiakili 17
Kuzuiliwa kwa watu kwa madhumuni yanayokiuka maadili 17
Unyanyasaji wa kimapenzi – Watoto.....18
Uendelezaji au uhamasishaji wa makosa ya kimapenzi na watoto 18
Utalii wa ngono na watoto 18
Ukahaba wa watoto 18
Ulinzi kutokana na unyanyasaji wa kimapenzi 19
Ponografia ya watoto 19
Ghasia za kinyumbani – Watu wazima 20
Vitendo vinavyonuia kusababisha madhara makubwa 20
Madhara makubwa 20
Kulisha sumu kimakusudi kwa nia ya kudhuru (Sehemu ya 236 ya Utaratibu wa Adhabu) 20

Kujeruhi au kulisha sumu kinyume cha sheria 20
Shambulio la kawaida 20
Shambulio linalosababisha madhara ya kimwili 20
Ghasia za Kinyumbani — Watoto 21
Ulinzi kutokana na dhuluma 21
Adhabu kwa ukatili na kutelekezwa kwa watoto 21
Ulanguzi — Watu wazima 22
Ulanguzi wa Watu 22
Uendelezaji au uhamasishaji wa ulanguzi wa watu 22
Kupatikana kwa hati za usafiri kwa njia ya udanganyifu au kupotosha (Sehemu ya 6 ya Kifungu cha sheria kinachopinga Ulanguzi wa Watu 2010) 23
Kurahisisha kuingia au kutoka nchini (Sehemu ya 7 ya Kifungu cha sheria kinachopinga Ulanguzi wa Watu 2010) 23
Hali za kutishia maisha au kifo 23
Ulanguzi wa watu kwa uhalifu uliopangwa 23
Ulanguzi — Watoto 24
Vitendo vinavyoendeleza ulanguzi wa watoto 24
Mila za kitamaduni zinazosababisha madhara 24
Utekelezaji wa sheria kuhusiana na hatia zinazohusisha nchi nyingine. 24
Makosa ya ukeketaji 24
Kusaidia na kushirikiana katika ukeketaji 24
Kulipa mtu kutekeleza ukeketaji katika nchi nyingine (Sehemu ya 21 ya Kifungu cha sheria kinachopinga marufuku Ukeketaji 2011) 25
Utumiaji wa nyumba au makazi kutekeleza ukeketaji 25

Umiliki wa vifaa na vyombo vya kutekeleza ukeketaji 25
Kushindwa kutoa ripoti ya utendaji wa kosa 25
Utumiaji wa lugha ya kushusha hadhi au ya matusi 25
Ulinzi kutokana na tambiko za kimila zinazosababisha madhara 26
Unachopaswa kufanya iwapo utakuwa mwathiriwa wa ubakaji/jaribio la ubakaji/unajisi/jaribio la unajisi au kosa lingine lolote la dhuluma ya kimapenzi? 26
Hifadhi Ushahidi 27
Unachopaswa kufanya ukiwa mwathiriwa wa mila za kitamaduni zinazosababisha madhara au kujua mtu ambaye ni mwathiriwa wa mila za kitamaduni zinazosababisha madhara? 27
Unachopaswa kufanya ikiwa umekuwa mwathiriwa wa ulanguzi au unafahamu mtu ambaye ameathiriwa na biashara hiyo ya ulanguzi? 27
Nambari za kupiga ukitaka kutoa ripoti 28

Utangulizi

Wanaotekeleza ghasia za kijinsia (GBV) mara nyingi huwa wale walio na uhusiano wa karibu na waathiriwa kama vile waume au wapenzi, watu wa familia, jamaa wa karibu, marafiki, wanachama wa jamii, maafisa wa usalama na hata wafanyakazi wa utoaji misaada. Katika visa vingi vya ghasia za kijinsia, waathiriwa hawatafuti usaidizi wala kuzungumzia jambo hilo kutokana na hofu ya unyanyapaa au kubaguliwa na jamii zao wenyewe au wakati mwingine kwa sababu hawafahamu haki zao. Hii husababisha waathiriwa kijihukumu wenyewe na vizazi vyao vijavyo kuendelea kuwa na maisha ya dhuluma, ghasia na ukosefu wa usawa.

Ubia wa wakimbizi nchini Kenya (RCK) umetayarisha kijitabu hiki kama kifaa muhimu cha utoaji habari na maelezo kuhamasisha wakimbizi na wanaotafuta hifadhi nchini kuwasaidia kuelewa ghasia za kijinsia ni nini, jinsi ya kutambua na kuzizuia katika jamii, kuwahamasisha kuhusu haki zao na hatua za kujilinda kulingana na sheria mbalimbali za Kenya (kwa mfano Kifungu cha sheria kuhusu Dhuluma za Kimapenzi 2006, Kifungu cha sheria kinachopiga marufuku Ukeketaji 2011, Kifungu cha sheria kinachopinga Ulanguzi wa Watu 2010, Sheria ya Watoto 2001 na Utaratibu wa Adhabu nchini Kenya), na kuwapa uwezo wa kuelewa na kujibadilisha kukomesha ghasia za kijinsia katika jamii wanamoishi.

Ili kurahisisha usomaji masuala yaliyomo yamewekwa katika mada tano muhimu, ambazo ni ghasia za kimapenzi, unyanyasaji wa kimapenzi, ghasia za kinyumbani, ulanguzi na mila za kitamaduni zinazosababisha madhara. Kila mada imegawanywa katika sehemu inayotoa Sheria za Kenya zinazolinda watu wazima na watoto.

Dhana Muhimu

Uke/ume yaani **Sex** kwa kiingereza inamaanisha maumbile ya kibiologia ya kimwili ambayo hayawezi kubadilishwa. Hii ni kutokana na tofauti ya jinsia ya kiume, kike na wetu wenye jinsia mbili ambayo inaamuliwa wakati wa kuzaliwa na ni sawa katika kila jamii.

Jinsia yaani **gender** kwa kiingereza inaashiria tabia au sifa za kijamii na kitamaduni zilizopewa wanaume na wanawake kwa mfano majukumu, hadhi na uhusiano wa mamlaka. Watu huendelea kujifunza sifa hizo katika maisha yao yote na zinaweza kubadilika kulingana na wakati, tamaduni na mazingira. Jinsia ya mtu humtofautisha mtu kuambatana na mtazamo wa jamii kuhusiana na maumbile fulani na jukumu yanayotekelezwa au yanayotarajiwa kutekeleza (kiume na kike).

Mfano mmoja wa jinsia/jukumu la jinsia ni ile taswira ya kawaida ya mwanamme kuchukuliwa kuwa mkimu familia naye mwanamke kuwa mtunzaji wa nyumba. Ni kwa sababu ya dhana tofauti za jinsia kwamba katika kila jamii na tamaduni, wanawake na wanaume wana nafasi tofauti na wanashiriki kwa njia tofauti katika masuala ya kikundi hicho.

Dhuluma ni utumiaji mbaya wa mamlaka ambapo mtekelezaji anapata na/au kudumisha udhibiti au kumtumia mwathiriwa kujinufaisha kwa kutumia na kusababisha madhara ya kimwili na kisaikolojia au hofu ya madhara hayo. Dhuluma humzuia mtu kufanya uamuzi huru na kuwalazimisha kufanya mambo yaliyo kinyume cha matakwa yao.

Mtoto ni binadamu yeyote aliye na umri wa chini ya miaka 18.
Kibali au idhini ni uchaguzi ambao mtu anaufanya baada ya kupata habari kamili kuhusu jambo fulani, ambao ni huru na wa hiari. HAKUNA kibali iwapo mtu atashawishiwa kufanya jambo baada ya kutishwa, kulazimishwa au kushurutishwa, kutekwa nyara, udanganyifu, kupewa habari za uongo kama ukweli au fasiri ya uongo kama sahihi. Kibali pia hakiwezi kutolewa na mtu aliye chini ya umri unaokubalika kisheria wa miaka 18.

Unajisi ni kitendo ambacho kinasababisha ngono na mtoto au mtu yeyote anayechukuliwa kuwa hana uwezo wa kuelewa hali ya kitendo cha ngono na hivyo basi hawezi kutoa kibali.

Ghasia za kinyumbani ni kitendo chochote cha ghasia za kimwili, kimapenzi, kisaikolojia na kiuchumi ambacho kinatokea miongoni mwa familia au nyumbani, hata ikiwa anayetekeleza kitendo hicho haishi mahala hapo na waathiriwa.

Ubakaji ni kitendo cha kimapenzi kinachosababisha ngono na mtu mwingine yeyote bila idhini yake.

Unyanyasaji wa kimapenzi ni aina ya dhuluma ya kimapenzi inayohusisha kutumia hila au shuruti kuwaingiza watu kwenye shughuli za ngono ili kujinufaisha au kupata bidhaa na hii hufanyika wakati kunapokuwa na ukosefu wa usawa wa mamlaka, jambo ambalo humwacha mwathiriwa na hiari finyu ya kujua la kufanya.

Ulanguzi ni kitendo cha mtu kuandikisha, kusafirisha, kuhamisha, kuweka au kupokea mtu mwingine kwa lengo la kumnyanyasa.

Ghasia ni madhara ya kimwili, kiakili, kijamii au kiuchumi. Baadhi ya aina za ghasia hujumuisha utumiaji wa dhuluma.

Ghasia za Kijinsia ni Nini?

Ghasia za kijinsia (GBV) zinaelezewa kuwa ghasia ambazo zinafanywa dhidi ya mtu fulani kwa misingi ya jinsia yake. Kwa kawaida ghasia za kijinsia hufanywa na wanaume dhidi ya wanawake na wasichana na zinatokana na misingi ya kihistoria ya kutokuwepo usawa wa uhusiano wa mamlaka baina ya wanaume na wanawake. Hali hiyo husababisha kutawaliwa na kubaguliwa dhidi ya wanawake na wanaume na kuzuia kuendelea kikamilifu kwa wanawake. Ghasia dhidi ya wanawake ni mojawapo ya njia ambazo wanawake hulazimishwa kuwa katika nafasi ya chini wakilinganishwa na wanaume.

Hata ingawa wanawake na wasichana ndio waathiriwa wakubwa wa ghasia za kijinsia, kuna uwezekano kwa wanaume na wavulana pia kuwa waathiriwa na haswa mashoga au watu wengine wanaoonekana kuwa hawatimizi kanuni dhahiri za kijinsia kuambatana na majukumu yaliyoamuliwa na jamii, matarajio na tabia.

Wakimbizi, na kwa kiwango fulani watu waliopoteza makao nchini kama kundi la wahamiaji waliolazimika kuhama, ni miongoni mwa watu wanaothiriwa kwa urahisi na vitendo vya ghasia za kijinsia.

Aina za Ghasia za Kijinsia

Ghasia za kimapenzi

Ni kitendo chochote cha mapenzi kinachotekelezwa au jaribio kufanywa dhidi ya mtu ambaye hajatoa idhini, au mtu ambaye hana uwezo wa kukubali au kukataa kuruhusu kitendo hicho. Zinajumuisha ubakaji, unajisi, kujamiiana kwa maharimu, ulawiti, dhuluma za kimapenzi, unyanyasaji wa kimapenzi, ukahaba wa lazima na bugudha za kimapenzi.

Ghasia za kimwili

Ni utumiaji wa nguvu za kimwili kwa nia ya kusababisha madhara. Unajumuisha mashambulio ya nguvu, kuchapwa, kupigwa mateke, kulemazwa, kuchomwa, ulanguzi na utumwa.

Ghasia za kihisia na kisaikolojia

Ni mwenendo wowote unaomfanya mtu mwingine kujihisi kila mara mwenye huzuni, kudhalilishwa, kuaibishwa, kuwa na hofu au kufadhaika au kujihisi kutofaa. Zinajumuisha matusi yanayodunisha, kushusha hadhi, kunyima fedha za kimsingi kwa familia kujikimu maishani, kuzuiliwa (kumtenga mtu kutoka kwa marafiki au familia au kuzuia mienendo yake).

Ghasia za kijamii na kiuchumi.

Ni kule kumzuia mtu kupata elimu, usaidizi wa kiafya, pesa, kazi, ardhi na hati za kibinafsi.

Mila za kitamaduni zinazosababisha madhara

Hizi zinaashiria aina za ghasia ambazo zinatekelezwa dhidi ya wanawake na wasichana katika jamii fulani na zinachukuliwa kuwa sehemu ya mila za kitamaduni zinazokubalika. Mila hizi husababisha madhara ya kimwili na kisaikolojia, ulemavu, kiwewe na hata kifo. Mila kama hizo ni kinyume cha sheria kabisa nchini Kenya.

Zinajumuisha ukeketaji (FGM), ndoa za mapema, ndoa za kulazimishwa, kuua ili kutunukiwa heshima fulani, kulemaza, uuaji wa mtoto mchanga, kunyimwa elimu kwa wanawake na wasichana, kutekwa nyara kwa watoto na urithi wa kulazimishwa wa wajane.

Ukeketaji wasichana

Ukeketaji (FGM) ni tohara ya kike, ambapo sehemu au viungo vyote vya uzazi vya mwanamke au msichana hutolewa, au viungo hivyo vya uzazi kujeruhiwa. Mila hii hutekelezwa kwa mwanamke au msichana wa umri wowote lakini kitamaduni inalenga wale wa umri mdogo, kutoka punde tu baada ya kuzaliwa hadi miaka ya ujana.

Aina yoyote ya ukeketaji imepigwa marufuku nchini Kenya. Haijalishi ikiwa mtu aliyekeketwa alikubali kufanyiwa tohara hiyo au alitoa idhini.

Wakimbizi nchini Kenya wanalindwa vipi kutokana na ghasia za kijinsia?

Mkimbizi yeyote au mtu anayetafuta hifadhi nchini Kenya anapewa ulinzi sawa na mwananchi wa Kenya dhidi ya ghasia za kijinsia. Kenya ina vifungu kadhaa vya kisheria vilivyobuniwa kulinda yeyote anayeishi humu nchini kutokana na uhalifu huo. Sheria hizi zinajumuisha:

- Kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006;
- Kifungu cha sheria kinachopiga marufuku ukeketaji 2011;
- Kifungu cha sheria za watoto 2001;
- Kifungu cha sheria kinachozuia ulanguzi wa watu 2010;
- Sheria chini ya utaratibu wa adhabu;

Iwapo mkimbizi au mtu yeyote anayetafuta hifadhi ameteseka kutokana na ghasia za kijinsia, anapaswa kutoa ripoti ya kisa hicho kwa polisi. Baada ya hapo kisa hicho kitawasilishwa mahakamani ambapo mshtakiwa akipatikana na hatia ya kutekeleza kosa hilo atashtakiwa na kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria. Kwa vile sheria hizi ni muhimu katika kuwalinda wakimbizi na wanaotafuta hifadhi, ni muhimu wafahamu sheria na haki zao.

Ghasia za kimapenzi – Watu wazima

Ubakaji (Sehemu ya 3 ya Kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006)

Mtu anatekeleza ubakaji anaposababisha ngono (uume unapoingia kwenye uke) na mtu mwingine kwa makusudi lakini bila idhini ya mtu huyo mwingine.

Adhabu: Kifungo cha muda usiopungua miaka 10 au hadi kifungo cha maisha.

Jaribio la ubakaji (Sehemu ya 4 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006)

Mtu anayejaribu kufanya ngono na mtu mwingine bila idhini yake ana hatia ya kosa la jaribio la ubakaji.

Adhabu: Kifungo cha muda usiopungua miaka 5 au hadi kifungo cha maisha.

Shambulio la nguvu la kimapenzi (Sehemu ya 5 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006)

Ikiwa mtu ataingilia sehemu za siri za mtu mwingine akitumia sehemu za mwili za mtu mwingine, kifaa au ikiwa atalazimisha mtu kutumia sehemu zake za mwili mwenyewe kujiingilia kingono bila idhini ya huyo mtu mwingine basi atakuwa na hatia ya kosa la shambulio la nguvu la kimapenzi.

Adhabu: Kifungo kisichopungua miaka 10 au hadi kifungo cha maisha.

Vitendo vya kuaibisha vilivyolazimishwa au kushawishiwa (Sehemu ya 6 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006)

Vitendo vya kuaibisha vinajumuisha: kushika kimakusudi sehemu za siri, matiti au matako ya mtu mwingine, lakini hakuna kuingilia kingono au kulazimisha mtu yeyote kutizama picha za ponografia za kutia ashiki. Mtu anayelazimisha au kusababisha mtu mwingine kushiriki kwenye kitendo cha kuaibisha bila kibali cha mtu huyo mwingine na:

- Mtu mwenyewe;
- Mtu huyo mwingine;
- Mtu mwingine wa tatu;
- Kifaa;
- Mnyama.

Ambacho mtu huyo asingefanya, kuruhusu au kuelewa ana hatia ya kosa hilo.

Adhabu: Kifungo cha muda usiopungua miaka 5.

Vitendo vinavyosababisha kuingilia kingono au vitendo vya kuaibisha mbele ya familia, watoto au wale wenye ulemavu wa kiakili **(Sehemu ya 7 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006)**

Mtu anayetekeleza kosa la ubakaji au kitendo cha kuaibisha kimakusudi huku akiruhusu mtu wa familia, mtoto au mtu mwenye akili punguani kutizama kitendo hicho ana hatia ya kosa hilo.

Adhabu: Kifungo cha muda usiopungua miaka 10.

Unajisi wa watu wenye akili punguani na mazuzu (Sehemu ya 146 ya Utaratibu wa Adhabu)

Mtu anayefanya ngono au kujaribu kufanya ngono na mtu anayefahamu kuwa ana ulemavu wa kiakili (lakini hatekelezi ubakaji) ana hatia ya kutenda uhalifu.

Adhabu: Kifungo kikiandamana na kazi ngumu kwa miaka 14.

Vitendo vya kuaibisha na watu wazima (sehemu ya 11A ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006)

Mtu anapotekeleza kitendo cha kuaibisha na mtu mzima bila idhini yake ana hatia ya kufanya uhalifu huo.

Adhabu: Kifungo kisichozidi miaka 5 na/au faini ya hadi shilingi 50,000.

Bugudha za kimapenzi (Sehemu ya 23 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006)

Mtu yeyote mwenye uwezo/ udhibiti/mamlaka ambaye anatoa mapendekezo ya kimapenzi au kuitisha fadhila ya kimapenzi, ambayo anajua kwamba haitakikani ana hatia ya kosa la bugudha za kimapenzi.

Adhabu: Kifungo kisichopungua miaka 3 na/au faini ya kiasi kisichopungua shilingi 100,000.

Kuambukiza kimakusudi virusi vya ukimwi (HIV) au magonjwa mengine ya zinaa yanayotishia maisha (Sehemu ya 26 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006)

Mtu yeyote anayefahamu kwamba ameambukizwa virusi vya ukimwi au ugonjwa mwingine wowote wa zinaa unaotishia maisha na anayefanya lolote kimakusudi ambalo:

- Litaambukiza mtu mwingine;
- Litalete uwezekano wa mtu mwingine kuambukizwa;

Ana hatia kulingana na sehemu hii ya sheria hata ikiwa yeye ameoa au kuolewa na mtu huyo mwingine.

Adhabu: Kifungo cha muda usiopungua miaka 15 hadi kifungo cha maisha.

Kusambaza magonjwa (kifungu cha 186 cha Utaratibu wa Adhabu)

Mtu yeyote ambaye atasambaza ugonjwa unaotishia maisha huku akiwa anajua ana hatia ya kosa.

Mifano ya magonjwa mengine ya zinaa ya kuambukiza ni:

- Kisonono
- Kaswende
- Ugonjwa wa ini wa hepatitis b na c
- Chunjua za sehemu za uzazi (genital warts)
- Ugonjwa unaoambukizwa na viini vya bakteria unaofahamika kama chlamydia.

Adhabu: Kifungo cha hadi miaka 2 na/au faini.

Majaribio ya kutoa mimba mtu mwingine (Sehemu ya 158 ya Utaratibu wa Adhabu)

Mtu yeyote anayejaribu kusababisha utoaji mimba ya mwanamke, awe mja mzito au la, ana hatia ya kufanya kosa.

Adhabu: Kifungo cha miaka 1

Ghasia za kimapenzi - Watoto

Unajisi (Sehemu ya 8 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006)

Mtu yeyote anayesababisha ngono na mtoto ana hatia ya kosa la unajisi. Mtu huyo hatakuwa na hatia iwapo:

- Inaweza kuthibitishwa kwamba mtoto huyo amemfanya mshtakiwa kuamini kwamba yeye ana umri wa zaidi ya miaka 18;
- Mshtakiwa aliamini kwa kweli kwamba mtoto huyo alikuwa na umri wa zaidi ya miaka 18.

Hii itaamuliwa kwa kuzingatia hali zote ikiwa ni pamoja na hatua ambazo mshtakiwa alichukua kukadiria umri wa mtoto huyo. Ikiwa mtu aliyeshtakiwa ana umri wa chini ya miaka 18, mahakama inaweza kumshtaki mtu huyo kulingana na Kifungu cha sheria ya watoto au Kifungu cha sheria za taasisi ya wafungwa wenye umri mdogo (The Borstal Institutions Act).

Adhabu:

- **Ikiwa mtoto ana umri wa miaka 11 au chini: kifungo cha maisha**
- **Ikiwa mtoto ana umri wa kati ya miaka 12 na 15: kifungo kisichopungua miaka 20**
- **Ikiwa mtoto ana umri wa kati ya miaka 16 na 18: kifungo kisichopungua miaka 15.**

Jaribio la Kunajisi

(Sehemu ya 9 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006) Mtu anayejaribu kufanya kitendo kinachosababisha ngono na mtoto ana hatia ya jaribio la kunajisi.

Adhabu: Kifungo cha muda usiopungua miaka 10.

Njama ya Kunajisi

(Sehemu ya 157 ya Utaratibu wa Adhabu) Kundi la watu ambalo linamfanya mwanamke au msichana, mwanamume au mvulana kupitia udanganyifu kufanya mapenzi na mtu mwingine ana hatia ya kufanya kosa.

Adhabu: kifungo cha miaka 3.

Kitendo cha kuaibisha na mtoto

(Sehemu ya 11 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006) Mtu anayetekeleza kitendo cha kuaibisha na mtoto ana hatia ya uhalifu. Mtu huyo hatakuwa na hatia iwapo:

Inaweza kuthibitishwa kwamba mtoto huyo alimfanya mtu huyo kuamini kwamba ana umri wa zaidi ya miaka 18; Mshtakiwa aliamini kwa kweli kwamba mtoto huyo alikuwa na umri wa zaidi ya miaka 18.

Adhabu:

- **Kifungo cha muda usiopungua miaka 10**
- **Ikiwa mtu aliyeshtakiwa ana umri wa chini ya miaka 18 anaweza kuhukumiwa kulingana na kifungu cha sheria cha wafungwa wa umri mdogo cha Bortal Institutions na kifungu cha sheria ya Watoto.**

Ikiwa mtu aliyeshtakiwa ana umri wa chini ya miaka 12 hatapatikana na hatia ya kitendo cha kuaibisha na mtoto.

Unyanyasaji wa Kimapenzi – Watu wazima

Unyanyasaji wa Ukahaba (Sehemu ya 17 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006)
Mtu yeyote anaye:

- Lazimisha kimakusudi au kusababisha mtu mwingine kuwa kahaba;
- Kudhibiti shughuli za mtu mwingine ambaye ni kahaba ili kumnufaisha yeye au mtu mwingine wa tatu;

Ana hatia ya kosa hili.
Adhabu: Kifungo kisichopungua miaka 5 na/au faini ya shilingi 500,000.

Ukahaba wa watu wenye ulemavu wa kiakili (Sehemu ya 19 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006)
Mtu au kampuni ambaye:

- Kwa sababu ya pesa au faida nyingine au fadhila anamlazimisha mtu mwenye ulemavu wa kiakili kushiriki katika ukahaba;
- Safirisha au kupokea mtu mwenye ulemavu nje ya mpaka akijua kwamba watatumiwa kutekeleza makosa ya kimapenzi;
- Anapiga chapa au kuchapisha picha au vitu vyovyote vinavyohimiza makosa ya kimapenzi dhidi ya mtu mlemavu;

Ana hatia kulingana na sehemu hii.
Adhabu: Kifungo kisichopungua miaka 10 na/au faini isiyopungua shilingi milioni 2.

Kuzuiliwa kwa watu kwa madhumuni yanayokiuka maadili (Sehemu ya 151 ya Utaratibu wa Adhabu)

Mtu yeyote anayemzuilia mtu kinyume cha matakwa yake ili kufanya naye ngono kinyume cha sheria ana hatia ya kosa.
Adhabu: Kifungo cha miaka 3 au zaidi au hukumu ya kifo.

Unyanyasaji wa kimapenzi – Watoto

Uendelezaji au uhamasishaji wa makosa ya kimapenzi na watoto (Sehemu ya 12 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006)

Mtu au kampuni ambaye:

- Anatengeneza au kugawa chochote kinachohimiza makosa ya kimapenzi na mtoto;
- Anawapatia au kuwaonyesha watoto vifaa vya ngono/makala yanayotumiwa katika vitendo vya ngono ili kumhimiza au ruhusu mtoto kufanya vitendo hivyo vya ngono ana hatia ya kosa hili.

Adhabu: Kifungo kisichopungua miaka 5 na ikiwa kampuni imeundwa kuendesha kosa hilo, faini isiyopungua shilingi 500,000.

Utalii wa ngono na watoto (Sehemu ya 14 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006)

Mtu au kampuni ambaye:

- Anatayarisha au kupanga usafiri kwa mtu (iwe ndani au nje ya Kenya) kwa nia ya kuandaa makosa ya kimapenzi dhidi ya mtoto hata ikiwa makosa ya kimapenzi hayatekelezwi;
- Anachapisha habari zinazohamasisha makosa ya ngono dhidi ya mtoto;
- Anatoa mawasiliano na mtu mwingine ambaye anahimiza makosa ya kimapenzi na mtoto;

Ana hatia ya kosa la utalii wa ngono.

Adhabu: Kifungo kisichopungua miaka 10 na ikiwa ni kampuni, faini isiyopungua shilingi milioni 2.

Ukahaba wa watoto (Sehemu ya 15 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006)

Mtu yeyote ambaye:

- Anaruhusu mtoto kuwa mahali ambapo anajua mtoto huyo atadhulumiwa kimapenzi au atashiriki katika tabia inayokiuka maadili;
- Anahimiza mtoto kujihusisha katika ngono au kushiriki katika maonyesho ya aina yoyote ya kuaibisha;
- Anamshawishi mtu yeyote kuwa mteja wa mtoto ili kushiriki ngono au maonyesho ya aina yoyote ya kuaibisha kupitia vyombo vya habari, matangazo ya mdomoni au njia nyingine sawa na hizo;
- Anachukua fursa ya uhusiano wake na mtoto kumfanya mtoto ashiriki ngono au dhuluma ya kimapenzi ya aina yoyote au maonyesho ya kuaibisha yanayokiuka maadili;

- Anaruhusu mali yake kutumiwa kwa makosa ya kimapenzi na mtoto;
- Analipia au kutoa manufaa mengine kwa huduma za kimapenzi za mtoto;

Anatenda kosa la kujinufaisha kutokana na ukahaba wa watoto.
Adhabu: Kifungo kisichopungua miaka 10.

Ulinzi kutokana na unyanyasaji wa kimapenzi (Sehemu ya 15 ya kifungu cha sheria ya watoto 2001)
Mtoto atalindwa dhidi ya kunyanyaswa kimapenzi na ukahaba, shughuli yoyote ya ngono na kuonyeshwa picha na vifaa chafu kimaadili. Mtu yeyote asiyeheshimu jukumu lake la kulinda mtoto anapaswa kuadhibiwa.
Adhabu: Kifungo cha hadi miezi 12 na/au faini isiyopungua shilingi 50,000.

Ponografia ya watoto (Sehemu ya 16 ya kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006)
Mtu yeyote au kampuni ambaye:
- Anauza, kukodisha, kusambaza, kuonyesha hadharani, kutoa au kumiliki vitabu vya ponografia, michoro, picha zilizochorwa, sanaa au kifaa kingine kichafu kimaadili chenye taswira au picha za mtoto;
- Anaagiza au kuuza nje ya nchi kifaa chochote cha ponografia chenye taswira au picha za mtoto;
- Anashiriki na kupata faida kutokana na biashara yoyote ambayo inajihusisha na ponografia ya watoto;
- Anatangaza au kufahamisha kwamba mtu ana hiari ya kufanya kitendo chochote ambacho ni hatia kwa mujibu wa sehemu hii;
- Anajitolea au kujaribu kufanya kitendo chochote ambacho ni hatia kulingana na sehemu hii;

Ana hatia ya kosa la ponografia ya watoto. Mtu huyo hana hatia iwapo:

- Chapisho hilo ni la manufaa kwa umma, linaendeleza sayansi, fasihi, mafunzo, au masomo mengine yanayohusu wote kwa ujumla;
- Litawekwa au kutumiwa kwa nia njema kwa madhumuni ya kidini;
- Linatambuliwa kama wasilisho la kisanaa kisheria
- Ni kitendo kati ya watu wawili walio na umri wa zaidi ya miaka 18.

Adhabu: Kifungo cha muda usiopungua miaka 6 na/au faini isiyopungua shilingi 500,000 au kifungo cha miaka 7 bila faini.

Ghasia za kinyumbani – Watu wazima

Vitendo vinavyonuiwa kusababisha madhara makubwa (sehemu ya 231 ya Utaratibu wa Adhabu)

Mtu yeyote ambaye kwa makusudi anajaribu kumuumiza au kumsababishia madhara makubwa mtu mwingine kwa njia yoyote ile ana hatia ya kosa na anaweza kufungwa gerezani maisha. Hii ni pamoja na kumchapa mtu au kumpiga mtu na kifaa cha aina yoyote.

Adhabu: Kifungo cha maisha

Madhara makubwa (Sehemu ya 234 ya Utaratibu wa Adhabu)

Mtu yeyote ambaye anaumiza au kumsababishia madhara makubwa mtu mwingine ana hatia ya kosa.

Adhabu: Kifungo cha maisha

Kulisha sumu kimakusudi kwa nia ya kudhuru (Sehemu ya 236 ya Utaratibu wa Adhabu)

Mtu yeyote anayemlisha sumu mtu mwingine akiwa na nia ya kumdhuru mtu huyo ana hatia ya kutenda kosa.

Adhabu: Kifungo cha miaka 14.

Kujeruhi au kulisha sumu kinyume cha sheria (Sehemu ya 237 ya Utaratibu wa Adhabu)

Mtu yeyote ambaye anamuumiza mwingine kinyume cha sheria au anamjeruhi kimakusudi kinyume cha sheria au anamkasirisha mtu yeyote au anampa mtu mwingine sumu ana hatia ya kutenda kosa hili.

Adhabu: Kifungo cha miaka 5.

Shambulio la kawaida (Sehemu ya 250 ya Utaratibu wa Adhabu)

Mtu yeyote anayempiga mwingine ana hatia ya kutenda kosa.

Adhabu: kifungo cha mwaka 1.

Shambulio linalosababisha madhara ya kimwili (Sehemu ya 251 ya Utaratibu wa Adhabu)

Mtu yeyote anayempiga mtu mwingine na kumuumiza ana hatia ya kufanya kosa hili.

Adhabu: Kifungo cha miaka 5.

Ghasia za Kinyumbani – Watoto

Ulinzi kutokana na dhuluma (Sehemu ya 13 ya kifungu cha sheria cha watoto 2001)

Mtoto ana haki ya kulindwa dhidi ya dhuluma za kimwili na kisaikolojia, kutelekezwa na aina nyingine yoyote ile ya unyanyasaji ikiwa ni pamoja na uuzaji, ulanguzi na utekaji nyara na mtu yeyote.

Adhabu: Kifungo cha hadi miezi 12 na/au faini ya kiasi cha hadi shilingi 50,000.

Adhabu kwa ukatili na kutelekezwa kwa watoto (Sehemu ya 127 ya kifungu cha sheria za watoto 2001)

Mtu yeyote ambaye ana jukumu la kuwa mzazi, mlezi, msimamizi au mwangalizi wa mtoto yeyote na ambaye:

- Kimakusudi anamshambulia, kumdhulumu, kumtelekeza au kumweka mtoto huyo katika hali ambayo inaweza kumdhuru, ikiwa ni pamoja na kumfanya kujeruhiwa, kupoteza uwezo wa kuona, kusikia, kiungo au sehemu ya mwili, na hali yoyote ile ya kuvuruga akili; au
- Kwa kitendo chochote au kwa kutofanya ipasavyo, kusababisha hali hatari kwa mtoto huyo na kumfanya ahitaji kulindwa;

Ametenda kosa.

Adhabu: Kifungo cha miaka isiyozidi 5 na/au faini ya shilingi 200,000.

Ulanguzi – Watu wazima

Ulanguzi wa Watu (Sehemu ya 3 ya Kifungu cha sheria kinachopinga Ulanguzi wa Watu 2010)

Mtu ana hatia ya ulanguzi wa watu ikiwa atasafirisha, kuandikisha, kuhamisha, kuweka au kupokea mtu mwingine baada ya:

- Kutishwa;
- Kumdanganya Au Kulaghai Mwathiriwa;
- Kumfanya Mtu Huyo Aamini Jambo Lisilo La Kweli;
- Kutumia Mamlaka Yao Vibaya Au Kuchukua Fursa Ya Udhaifu Wa Mwathiriwa Kumnyanyasa;
- Kupata Malipo Au Manufaa Kutoka Kwa Mwathiriwa Kwenye Biashara Hiyo Haramu.
- Bado ni kosa kulingana na kifungu hiki cha sheria ikiwa mwathiriwa wa ulanguzi ametoa kibali/amekubali kuhusishwa kwenye biashara hiyo haramu.
- Kuhamisha au kuweka mtoto ili kumnyanyasa pia ni ulanguzi wa watu ni uhalifu.
- Ulanguzi wa watu unaweza kufanywa ndani ya nchi ya Kenya au kimataifa.

Adhabu: Kifungo kisichopungua miaka 15 na/au faini isiyopungua shilingi milioni 5. Kosa likitokea tena: Kifungo cha maisha.

Uendelezaji au uhamasishaji wa ulanguzi wa watu (sehemu ya 5 ya Kifungu cha sheria kinachopinga Ulanguzi wa Watu 2010)

Mtu yeyote ambaye:

- anajua kwamba anakodisha nyumba yake, ardhi au mali nyingine yoyote na itatumiwa kusaidia au kuhimiza ulanguzi;
- anachapisha, anaagiza au kuuza nchi za nje, vifaa vyovyote kwa madhumuni ya kusaidia au kuhimiza ulanguzi wa watu;
- anasimamia, kuendesha au kulipia wakala kuhimiza au kusaidia ulanguzi wa watu;
- anahimiza au kusaidia ulanguzi kwa njia nyingine yoyote;

Anatenda kosa.

Adhabu: Kifungo kisichopungua miaka 10 na/au faini isiyopungua shilingi milioni 5. Ikiwa mtu huyo atarudia kosa hilo atafungwa kwa kipindi kisichopungua miaka 15.

Kupatikana kwa hati za usafiri kwa njia ya udanganyifu au kupotosha (Sehemu ya 6 ya Kifungu cha sheria kinachopinga Ulanguzi wa Watu 2010)

Mtu yeyote ambaye anayedanganya au kubuni matukio yasiyo ya ukweli au kutoa habari za uongo ili kupata hati za kusafiri kusaidia katika ulanguzi wa watu ana hatia ya kutenda kosa..

Adhabu: Kifungo kisichopungua miaka 10 na/au faini isiyopungua shilingi milioni 1.

Kurahisisha kuingia au kutoka nchini (Sehemu ya 7 ya Kifungu cha sheria kinachopinga Ulanguzi wa Watu 2010)

Mtu yeyote anayesaidia mwingine kuingia na kutoka nchini Kenya ili waweze kuendesha biashara haramu ya ulanguzi wa watu ana hatia ya kutenda uhalifu.

Adhabu: Kifungo kisichopungua miaka 10 na/au faini isiyopungua shilingi milioni 5.

Hali za kutishia maisha au kifo (Sehemu ya 9 ya Kifungu cha sheria kinachopinga Ulanguzi wa watu 2010)

Ikiwa mwathiriwa wa ulanguzi wa watu:

- Atapata Majeraha Ya Kudumu Au Madhara Ya Kimwili Au Afya Yake Kupata Madhara Kutokana Na Hali Zilizoweka Maisha Yao Hatarini; Au
- Mwathiriwa afariki kutokana na hali wakati wa ulanguzi huo;

Mtu ambaye ana hatia ya kuendesha biashara ya ulanguzi wa mtu huyo atahukumiwa kifungo cha maisha.

Adhabu: Kifungo cha maisha.

Ulanguzi wa watu kwa uhalifu uliopangwa (Sehemu ya 10 ya Kifungu cha sheria kinachopinga Ulanguzi wa Watu 2010)

Ikiwa mtu anayehusika na ulanguzi wa watu atapatikana kuwa sehemu ya kundi lililopangwa la uhalifu au kwamba walikuwa wanaelekeza kundi au genge hilo katika ulanguzi, watapatikana na hatia ya kosa hili na watahukumiwa kifungo cha maisha.

Adhabu: Kifungo cha maisha.

Ulanguzi – Watoto

Vitendo vinavyoendeleza ulanguzi wa watoto (Sehemu ya 4 ya Kifungu cha sheria kinachopinga Ulanguzi wa Watu 2010)

Mtu ambaye:

- Anapanga au kutoa mtoto apangishwe;
- Anachukua au kutoa mtoto kwa utunzi wa mlezi;
- Anakuwa mlezi au anatoa mtoto kwa mtu mwingine awe mlezi wake;

Kwa lengo la kufanya ulanguzi na mtoto huyo ana hatia ya kosa hili.

Adhabu: Kifungo kisichopungua miaka 15 na/au faini isiyopungua shilingi milioni 10. Kosa likirudiwa: Kifungo cha maisha.

Mila za kitamaduni zinazosababisha madhara Utekelezaji wa sheria kuhusiana na hatia zinazohusisha nchi nyingine (Sehemu ya 28 ya Kifungu cha sheria kinachopiga marufuku Ukeketaji 2011)

Wakati ukeketaji unapofanywa katika nchi nyingine na mtu yeyote ambaye ni raia wa Kenya au mtu ambaye sio Mkenya lakini anaishi nchini Kenya mtu huyo atahukumiwa kulingana na sheria za Kenya.

Adhabu kwa ukeketaji: Kifungo kisichopungua miaka 3 na/au faini isiyopungua shilingi 200,000.

Makosa ya ukeketaji (Sehemu ya 19 ya Kifungu cha sheria kinachopiga marufuku Ukeketaji 2011)

Mtu yeyote anayemfanyia ukeketaji mtu mwingine anatenda kosa (hawa ni pamoja na madaktari, wakunga, yeyote anayefanya mafunzo kuwa daktari).

Adhabu:

- **Kifungo cha miaka 3 au zaidi na/au faini isiyopungua shilingi 200,000.**
- **Iwapo mwathiriwa wa ukeketaji atafariki kutokana na kosa hilo adhabu itakuwa kifungo cha maisha.**

Kusaidia na kushirikiana katika ukeketaji (Sehemu ya 20 ya Kifungu cha sheria kinachopiga marufuku Ukeketaji 2011)

Mtu yeyote ambaye:

- Anasaidia katika kutekeleza shughuli hiyo; au
- Kuhimiza mtu kufanyiwa upasuaji huo; au
- Anaenda kufanyiwa ukeketaji mwenyewe;

Anatenda kosa kulingana na Kifungu hiki.

Adhabu: Kifungo cha miaka 3 au zaidi na/au faini isiyopungua shilingi 200,000.

Kulipa mtu kutekeleza ukeketaji katika nchi nyingine (Sehemu ya 21 ya Kifungu cha sheria kinachopiga marufuku Ukeketaji 2011) Iwapo mtu:

- Anampeleka mtu mwingine katika nchi nyingine (nje ya Kenya); au
- Anamleta mtu mwingine nchini Kenya kutoka nchi nyingine; ili mtu huyo apelekwe kwa tohara ya kike, mtu huyo ana hatia ya kutenda kosa.

Adhabu: Kifungo cha miaka 3 au zaidi na/au faini isiyopungua shilingi 200,000.

Utumiaji wa nyumba au makazi kutekeleza ukeketaji (Sehemu ya 22 ya Kifungu cha sheria kinachopiga marufuku Ukeketaji 2011)

Mtu yeyote anayeruhusu makao yake (nyumba, ofisi au ardhi) itumiwe kutekeleza tohara ya kike ana hatia ya kutenda kosa.
Adhabu: Kifungo cha miaka 3 au zaidi na/au faini isiyopungua shilingi 200,000.

Umiliki wa vifaa na vyombo vya kutekeleza ukeketaji (Sehemu ya 23 ya Kifungu cha sheria kinachopiga marufuku Ukeketaji 2011)

Mtu yeyote ambaye ana chochote (nyembe, visu, makasi, vioo vilivyopasuka au mawe yaliyochongwa) ambacho kitatumiwa kutekeleza tohara ya kike anatenda kosa.
Adhabu: Kifungo cha miaka 3 au zaidi na/au faini isiyopungua shilingi 200,000.

Kushindwa kutoa ripoti ya utendaji wa kosa (Sehemu ya 24 ya Kifungu cha sheria kinachopiga marufuku Ukeketaji 2011)
Mtu yeyote anayefahamu kwamba:

- Msichana au mwanamke anatahiriwa; au
- Mtu ametekeleza tohara ya kike; au
- Mtu anapanga kutekeleza ukeketaji;

Na anakosa au kushindwa kutoa ripoti kwa afisa wa polisi ana hatia ya kutenda kosa.

Adhabu: Kifungo cha miaka 3 au zaidi na/au faini isiyopungua shilingi 200,000.

Utumiaji wa lugha ya kushusha hadhi au ya matusi (Sehemu ya 25 ya Kifungu cha sheria kinachopiga marufuku Ukeketaji 2011)

Mtu yeyote anayefanya mzaha kwa njia ya kuchukiza au kuudhi dhidi ya msichana au mwanamke ambaye hajatahiriwa au mwanamume anayemuoa mwanamke ambaye hajatahiriwa ili wafedheheshwe katika jamii anatenda kosa.
Adhabu: Kifungo cha kipindi kisichopungua miezi sita na/au faini isiyopungua shilingi 50,000.

Ulinzi kutokana na tambiko za kimila zinazosababisha madhara (Sehemu ya 14 ya Kifungu cha sheria za watoto 2001)

Mtu yeyote anayemfanya mtoto kufanyiwa tohara ya kike, kuozwa mapema au taratibu nyingine yoyote ya kitamaduni na kimila ambayo itadhuru maisha, afya, hadhi, ukuaji wa kimwili au kisaikolojia wa mtoto huyo atakuwa ametenda uhalifu.

Adhabu: Kifungo cha hadi miezi 12 na/au faini ya hadi shilingi 50,000.

Kujamiiana kwa maharimu (Sehemu ya 20, 21 na 22 ya Kifungu cha sheria kuhusu dhuluma za kimapenzi 2006)

Kujamiiana kwa maharimu (incest) kunakotekelezwa na wanaume

Mwanamume yeyote ambaye anatekeleza kitendo ambacho kinasababisha kuingilia kingono au kujaribu kuingilia kingono mtu ambaye anajua kwamba ni binti yake, mjukuu wa kike, dada, mama, mpwa, shangazi au nyanya ana hatia ya kujamiiana kwa maharimu. Mtu huyo wa kike ataondolewa kutoka kwa utunzi wa mwanamume huyo.

Kujamiiana kwa maharimu (incest) kunakotekelezwa na wanawake

Mwanamke anayetekeleza kosa la kujamiiana kwa maharibu au kujaribu kutekeleza kosa hilo dhidi ya mwanamume ambaye anajua ni mwanawe wa kiume, baba, mjukuu wa kiume, babu, kaka, mpwa wa kiume, mjomba au binamu atakuwa na hatia ya kosa hilo. Kumbuka: Kaka na dada wanajumuisha kaka wa kambo na dada wa kambo, dada na kaka wa kupanga, na baba anajumuisha baba na mjomba wa karibu ilhali mama anajumuisha mama mdogo na shangazi wa karibu iwe ni kupitia ndoa ya kisheria au la.

Adhabu:

- **Kujamiiana kwa maharimu – kifungo cha maisha hata ikiwa mtu huyo mwingine ametoa kibali.**
- **Jaribio la kujamiiana kwa maharimu – kifungo kisichopungua miaka 10.**

Unachopaswa kufanya iwapo utakuwa mwathiriwa wa ubakaji/jaribio la ubakaji/unajisi/jaribio la unajisi au kosa lingine lolote la dhuluma ya kimapenzi?

Hifadhi Ushahidi

Ili kuonyesha kwamba kosa la dhuluma ya kimapenzi kwa kweli lilitekelezwa, ni muhimu kuonyesha ithibati au thibitisho kama vile ushahidi wa kimatibabu, ushahidi wa mahakama au hata kukiri kwa mshtakiwa.

Jinsi ya kuhifadhi ushahidi:

- Usioge au kufua nguo zako;
- Usiweke nguo zako kwenye mfuko wa plastiki, badala yake ziweke kwenye karatasi ya kaki inayotumiwa kufungia vitu au kwenye mfuko wa karatasi;
- Toa ripoti katika hospitali ya serikali iliyo karibu na kuitisha ripoti iliyoandikwa kuhusu kilichopatikana baada ya uchunguzi wa kimatibabu;
- Piga ripoti kwa kituo cha polisi kilicho karibu na kuitisha ripoti ya polisi iliyoandikwa na kutiwa sahihi.

Unachopaswa kufanya ukiwa mwathiriwa wa mila za kitamaduni zinazosababisha madhara au kujua mtu ambaye ni mwathiriwa wa mila za kitamaduni zinazosababisha madhara?

- Nenda katika hospitali kupata huduma ya matibabu na kupata ushahidi (ripoti iliyoandikwa kuhusu majeraha na uchunguzi wa kimatibabu);
- Piga ripoti ya kisa hicho kwa polisi.

Unachopaswa kufanya ikiwa umekuwa mwathiriwa wa ulanguzi au unafahamu mtu ambaye ameathiriwa na biashara hiyo ya ulanguzi?

- Toa ripoti ya kisa hicho kwa polisi.

Nambari za kupiga ikiwa kuna ripoti

Waathiriwa wa UWAKI wanaweza kutafuta Usaidizi kutoka kwa Washirika wafuatao

- **RCK** Toll Line: 0800720868
- **KNCHR Toll Line:** 0800720627
- **1195** Kenya's National GBV Hotline
- **1199** Kenya Redcross Toll Free Hotline
- **1517**-UNHCR Toll-Free Help Line
- **999/112** - Kenya Police Emergency Hotline 116 Child Help Line

Nambari za bila malipo:

- **112** (from mobile phone)
- **999** (from landline)
- **116** (children survivors hotline)

Simu zinazolipishwa:

- 0711400506 or 0733500101 **(Medicins sans Frontière hotline)**
- 020 208 8060/2088067 or 0733 860 669/ 0720 943 164 **(RCK Nairobi)**
- 0716 169 407/0719 297 750 **(RCK Dadaab)**
- 0719 297 950 **(RCK Kakuma)**
- 0719 605 493 **(RCK Garissa)**

JINSI YA KUWASILIANA NASI

Refugee Consortium of Kenya
S.L. Posta: 25340 - 00603, Nairobi, Kenya
Barua Pepe; info@rckkenya.org | Tovuti: www.rckkenya.org

Ofisi Kuu, Kilimani, Nairobi:
Haki House, Ndemi Road, Kilimani.
Nambari ya Simu: +254720943164, +254703820361
Laini Isiyohitaji Malipo: 0800720868

Ofisi ya Dadaab :
Nambari ya Simu: +254 703 848 641, 0705 862 534
S.L. Posta: 28, Dadaab, Kenya
Laini Isiyohitaji Malipo: 0800721692

Ofisi ya Kakuma :
Nambari ya Simu: +254 701 414 978
Laini Isiyohitaji Malipo: 0800720262

Ofisi ya Garissa na Mwingi :
Nambari ya Simu: +254 700 865 559

Ofisi ya Mombasa:
Nambari ya Simu: +254728569283

Nambari ya simu ya msaada ya UNHCR Kenya isiyohitaji malipo: 1517

Kurasa Zetu za Mitandao ya Kijamii :

@RCKKenya| @Refugee Consortium of Kenya – RCK|
@Refugee Consortium of Kenya – RCK
@rckkenya| @rckkenya| @RCK-kenya